Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 237 | SHAWAL-DHUL QA.1444AH | MEI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

Hadhi na Utukufu wa Kurani Tukufu

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu



Muhtasari wa Hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano[atba] iliyotolewa katika Masjid Mubarak, Uingereza siku ya Tarehe 10 Machi 2023

Ubora wa Kurani Tukufu – Ufasaha na Miujiza ya Mwongozo Kamili:

Baada Ya Kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba amekuwa akizungumzia ubora na uzuri wa Qur'ani Tukufu, na ataendelea na maelezo haya katika hotuba ya leo pia.

Mwongozo Kamili kwa Waamchao Mwenyezi Mungu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba Qur'ani Tukufu ni kitabu kamili na hakuna maandiko mengine yanayoweza kulinganishwa nayo. Katika surah ya kwanza ya Qur'ani Tukufu, Mwenyezi Mungu Anafundisha maombi 'Utuongoze kwenye njia iliyonyooka'. Sio kwamba hii ni dua tu, bali pia ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba kwa kufuata mafundisho ya Qur'ani Tukufu, mtu anaweza kuongozwa kwenye njia sahihi. Vile vile Mwenyezi Mungu Anabainisha jinsi lengo hili linavyoweza kufikiwa kwa kueleza katika surah ya pili ya Qur'ani Tukufu kwamba Kitabu hiki ni 'mwongozo kwa waamchao Mungu'.

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba ujio wa Mtume Mtukufu (saw) ukawa katika wakati ambapo hali za ulimwengu zilihitaji ujio wake, na matokeo ya ujio wake yalikuwa ni 'Leo Nimewakamilishieni dini yenu'. Ukamilifu haumaanishi tu kuteremshwa kwa aya, bali pia unahusu utakaso wa nyoyo na ukamilisho wa nafsi kwa wale wanaotekeleza na kufuata mafundisho ya Qur'ani Tukufu. Ilikuwa hivyo kwamba watu wa porini waligeuzwa kuwa watu wa khulka njema na watu hao wenye khulka njema kisha wakageuzwa kuwa watu wa kiroho. Hivyo, Qur'ani Tukufu iliwaleta watu kwenye ukamilifu huo, kama vile Kitabu cha Mwenyezi Mungu kilivyofikishwa kwenye ukamilifu. Hakuna ukweli au uhakika wowote ulioko nje ya upeo wa Qur'ani Tukufu.

Kitabu Pekee Kinachojumuisha Ukweli wote na Haki zote:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba anasoma Biblia na akagundua kwamba mafundisho ambayo Wakristo wanajivunia kwayo, kwa kweli yamefafanuliwa mfululizo na kikamilifu ndani ya Qur'ani Tukufu. Ni aibu kwamba Waislamu hawaitafakari Qur'ani Tukufu, kwa kuwa hakuna kitu kinachoweza kulingana nayo.

Hudhur (atba) alizidi kumnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba kwa hivyo, 'Leo Nimewakamilishieni dini yenu' ina maana kwamba mwanadamu amefikishwa hadi umbo lake la juu kabisa au ukamilifu wake na kwamba Qur'ani Tukufu imekamilishwa. Wakati Aya hii ilipoteremshwa, Myahudi mmoja alisema kwamba Waislamu waichukulie siku hiyo kuwa ni Eid. Hadhrat Umar (ra) akamjibu kwamba hii ilikuwa ni siku ya Eid, kwani ilikuwa ni Ijumaa.

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba Qur'ani Tukufu hadhi yake iko juu ya Hadithi (maneno ya Mtume

Endelea Uk wa 8..

Jamia Ahmadiyya Morogoro yatoa Zawadi ya Idd-ul-Fitr. Mh. Mkuu wa Mkoa Mgeni Rasmi.

Mh. Fatma Abubakar Mwassa

Na. Mwandishi wetu.



Endelea Uk wa 4..



Endelea Uk wa 5..

Ukinaifu ndani ya Ndoa uk. 03..

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kitabu na Hekima

Wanahasara kubwa wale wanaofikiria kwamba Dini ya Islam imeenezwa kwa upanga na watu wamelazimishwa kuingia katika Dini hiyo. Hao ni watu wa kuhurumia kwani hawajui lolote maskini kuhusu Islam. Vitabu vya historia hata hivyo vinatupa taswira tofauti. Katika Mwaka wanne wa Hijra, Mtukufu Mtume Muhammad saw aliweka sahini mkataba *wakuwalinda wahubiri, Mapadri, wakristo wa mtakatifu Catherine karibu na Mlima Sinai, katika mkataba huo kuna haya yafuatayo. ''Ni wajibu wa Waislamu kulinda Makanisa ya Wakristo na sehemu zao takatifu na kuwalinda dhidi ya adui yeyote yule. Wasitozwe kodi kiholela na wala wasilazimishwe kuondoka. Hakuna Mkristo atakaye lazimishwa kuacha dini yake. Hakuna kasisi atakaye ondolewa katika nyumba yake. Hakuna atakayekwenda kudhuru mahali patakatifu atakaye katazwa. Hakuna kanisa lolote litakalo bomolewa au kuwa mahali pakuishi kwa waislam au kuwa Msikiti. Ni wajibu kwa kila Mwislam kutoa misaada isiyo na masharti katika kuwasaidia Wakristo katika kujenga Makanisa na majengo yao mengine.*

Uso gani usiyo na aibu wa kumsingizia aliyeweka Saini hiyo kuwa aliwalazimisha watu kwa Upanga kuingia katika Islam. Ni aibu kwa wasomi wa ulaya. Ukweli ambao wanaufumbia macho ni kwamba Islam inasisItiza kuwa hakuna karaha katika Dini. Ushahidi usiyopingika ambao ni wazi Islam inasisitiza utumiaji wa akili, kitabu cha Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] *Falsafa ya Mafundisho ya Kiislam*, kina falsafa ya mafundisho ya Islam. Katika kitabu hiki ambacho kina nafasi ya aina yake katika Historia ya binadamu, Mafundisho ya Islam yameelezwa kwa Hekima kubwa mafunzo yote yamewekwa wazi. Sio wale wanaosema kuamini tu mengine wanayaita mafumbo. Hapa mafunzo yote yanaelezwa kinagaubaga. Binadamu amewekewa Uhuru wakukubali au kukataa falsafa inaelezwa kwanini mafunzo hayo yametolewa. Kurani Tukufu imekwenda sawa na maumbile, upo uhusiano mkubwa baina ya mwili na roho. Na kwa hakika roho haitoki nje bali inazaliwa kutoka ndani. Hivyo kuna uhusiano mkubwa baina ya mwili na roho.Katika falsafa ya nje yana athari na yaliyo ndani. Mfano ukicheka furaha inaonekana usoni, na unapo huzunika na huzuni unapenyeza kwenye moyo ndio maana katika Sala ya Kiislam unatakiwa utawadhe, kwani kutawadha kuna athari hata ndani. Unaposimama kwa unyenyekevu, ukainama na kusujudu. Vitendo hivyo vyote vina athiri moyo. Kwa hakika faida ya Sala ya KiiIslam licha ya kutoa shukrani kwa yote Wanasayansi wamethibitisha kuwa Sala ya Kiislam ni mazoezi tosha ya viungo. Tizama mantiki unapo katazwa chakula fulani kwa mathalani uzuri unapewa na sababu ukiambiwa kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani unaelezwa faida ya funga. Unapoambiwa kutekeleza ibada ya Hija unaelezwa pia faida Yake. ***Falsafa ya mafundisho ya Islam.*** Kweli ni sehemu ya pili ya ile ahadi yakutelemsha Kitabu na hekima ya mafundisho ya Islam haihitaji Upanga. Upanga mkali tu uonao ni Upanga wa hoja, hoja zinazo ingia akilini huku ukitikisa kichwa na kutabasamu. Huku kwetu hakuna mambo ya amini tu wala usiulize, hilo ni fumbo ,'' Huku kwetu mafumbo yote yamefumbuliwa. Ndio maana katika historia yetu yote hakuna mgongano wowote wa Quran Tukufu na Sayansi. Mgongano utatokea wapi wakati vitu hivi viwili vinatoka ofisi moja?



QUR'AN TUKUFU

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ)

Allah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wataniabudu hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio basi hao ndio wavunjao amri. (An-Nuur 24:56)

NUKUU YA HADITHI

Na **Ustadh Issa Malenge** - 0625 914 740 0752 334 332

حَدَّثَنَا مُسْلِمُ بْنُ إِبْرَاهِيمَ حَدَّثَنَا هِشَامٌ حَدَّثَنَا يَحْيَى عَنْ أَبِي سَلَمَةَ عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((مَنْ قَامَ لَيْلَةَ الْقَدْرِ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ، وَمَنْ صَامَ رَمَضَانَ إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ)).

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a ya kwamba Mtume s.a.w alisema:
Yule atakaye simama katika Usiku wa *Lailatul Qadir* Kwa imani na nia ya kupata thawabu Allah atamughofiria madhambi yake yote yaliyotangulia.
Na yule atakaye funga Ramadhani kwa Imani na nia ya kupata thawabu Allah atamghofiria Madhambi yake yote. (Bukhar).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[as]

Mahubiri ya Kiroho - 1

"*Wanazo habari njema katika maisha ya dunia*"
"*Kama mwanadamu mwenyewe asiwe mzembe katika kutafuta haki, Mungu mwenyewe amuongoza mtafuta kweli kwenye njia.*"

Jambo hili limethibitika ndani ya kurani na Hadithi ya Nabii mtukufu s.a.w kwamba mwaminio anaona ndoto njema zenye bishara na pia kwa ajili yake zinaonyeshwa kwa watu wengine. Hususan mwaminio katika mtazamo wa watu anapokuwa mwenye kukataliwa, kuachwa, kulaaniwa, kufukuzwa, kafiri, dajali bali kafiri mkubwa kuliko wote na mbaya kuliko wote, hapo katika wakati wa kusumbuka na kuvunjika moyo, Nani ayajuaye Yale maongezi yenye ladha na hisani yatokayo kwa Mwenyezi Mungu kuja kwa huyo mwaminio?

"Rehema ya Muumba iliyo kimbilio la mawalii, huwa inafichika chini ya laana za watu"Mimi siwezi kutoa shukurani ya hisani za Mwenyezi Mungu kwamba katika wakati huu wa kukufurishwa ambapo sauti za masheikh wa Zama hizi zinakuja toka kila upande kwamba "*wewe si mwaminio*" sauti kutoka kwa Mwenyezi Mungu ndiyo: "*Sema:Mimi nimetumwa, na ni wa Kwanza wa waaminio*". Upande mmoja masheikh wanasema kwamba mkomesheni kabisa mtu huyu kwa njia yoyote ile, na Upande mwingine nafunuliwa: "Wanakungojelea misiba,msiba mbaya uko juu yao."Na Upande mmoja wao wanajaribu kwamba mdhalilisheni kabisa mtu huyu na kumuondolea heshima,na Upande mwingine Mungu Anatoa ahadi:"*Mimi Nitamfedhehesha yule atakayetaka kukufedhehesha.Mwenyezi Mungu ndio ujira wako. Mwenyezi Mungu Atakupa ujalali wako.*" Na Upande mmoja masheikh wanaandika fatwa juu ya fatwa kwamba mtu akiwa na itikadi Kama ya mtu huyu au kwa kumfuata mtu huyu, anakua kafiri,na Upande mwingine Mwenyezi Mungu Anakazania kunifunulia Mara kwa Mara kuwa: "*Sema,ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni.*"Kwa ufupi, masheikh wote hawa wanapigana na Mwenyezi Mungu,Sasa tazameni ushindi anaupata nani.

Mwishoni iwe wazi kwamba kusudio langu katika maandishi haya ni hili kwamba baadhi ya watu toka panjab na India wameniletea kimaandishi ndoto zao nyingi walizotokewa na Mtume s.a.w na pia Ilhaam walizopata kuhusiana nami ambazo madhumuni yake takriban na Mara nyingi ni haya haya kwamba: Tumemuona Mtume s.a.w katika ruya au kwa njia ya ufunuo tumefahamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba mtu huyu, yaani **mimi**, anatoka kwa Mwenyezi Mungu,mkubalini.Hivyo ,baadhi yao walizieleza pia ndoto za aina hii kwamba Mtume s.a.w alionekana katika Hali ya kukasirika mno,na ilifahamika kuwa Kama vile ameketi nje ya kaburi takatifu akisema kwamba watu wote wa aina hii ambao kwa makusudi wanamsumbua mtu huyu, yaani **mimi** inakaribia wateremkiwe na ghadhabu ya Mungu.Mwanzoni sikuzitilia Sana maanani ndoto hizi, lakini sasa ninaona kwamba Jambo hili limeanza kutokea kwa wingi Sana duniani kiasi ya kwamba baadhi ya watu kutokana na ndoto tu wameacha uadui na chuki na kuingia katika kundi la waaminio waaminifu kamili,na kwa sababu hii hii wakaanza kutoa msaada wa Mali zao.

(Ishara ya Kimbingu uk 65-67)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ukinaifu ndani ya Ndoa

Na.



Maulana Sheikh
Shaban A. Shunda Sahib

...Kutoka toleo lililopita

Hivyo basi, sababu kubwa ya wanandoa kuchokana, au kuzeeka kwa ndoa kunasababishwa na mwanamke au mwanaume, pale ambapo atashindwa kutumia nafasi yake na vipawa alivyopewa kuleta utulivu katika ndoa yao, na hapa nitajaribu kujadili baadhi ya visababishi vinavyopelekea kuzeeka kwa ndoa au kuchokana visababishi ambavyo huwa vinadharaulika na kuonekana vitu vidogo vidogo hususan kwa wanawake wengi.

Tunasoma katika tamaduni za wenzetu Waarabu na Wahindi kwamba, mwanamke anapotaka kumvuta mumewe na kumpa ujumbe kuwa siku hio anamhitaji, basi hufanya usafi wa nyumba na hufukisha manukato nyumba nzima na pia kuandaa mazingira mazuri sehemu ya kulala na pia yeye mwenyewe akijivalia mapambo yake ya dhahabu hata kama yawe ni yale aliyovaa siku ya ndoa yao, ili muradi tu wanazingatia jambo hilo.

Uswahilini kwetu utapokewa na kijora kilicholowa jasho na pia harufu ya moshi wa jikoni alipokuwa anandaa chakula. Na mara zingine hatuna utaratibu wa kupokeana na kukumbatiana, wakati mmoja anapotoka nje iwe kwenye shughuli ama katika mizunguko ya kawaida. Mara kwa mara tunakutana na uzoefu wa mama yupo jikoni atakuja baada ya kumaliza kupika ama atokapo Mama Baba akiwepo nyumbani basi usitarajie kabisa makaribisho bali gubu la kwanini hivi kwanini vile, iwe Mama aulizwe kuchelewa au pia kama hana kosa la kupewa basi ataulizwa kwanini amekuja na boda boda huyu ili muradi wababa hatuna utaratibu wa kukaribisha wenzi wetu nyumbani.

Na kwa wanaume ni hatari mno kufanya nyumba kuwa ofisi, kwa namna hii kwamba baada ya kutoka katika mahangaiko basi ubebe kazi na kwenda kumalizia nyumbani, au uanze kupokea simu ndefu ndefu za biashara au kutokuwa sawa kwa sababu umekwazana na Mwajiri wako ofisini basi umsimulie mkeo au familia jinsi ulivyokwazika, inabidi ujue kujipanga kwamba ofisi ni ofisi na nyumbani ni nyumbani na uweze kutoa haki zao bila kunyima. Tujifunze kuwa sehemu tulipo kimawazo kifikira na uwepo hapo ndipo yalipo mafanikio hasa.

Katika kipindi hiki kitakacho wasaidia wanandoa ni ule umoja waliojijengea na urafiki wa karibu kwa sababu ni muda wa majukumu. Kama vile marafiki wanaweza wakakutana msibani wakajivuta kando na kupiga stori zao nje ya msiba na kuangua vicheko na kuburudika, basi hicho ndicho kitu kitakachofanya ndoa ipite salama katika wimbi hili, ifike kila mtu anasahau majukumu yake mazito na kutafutiana muda wa pamoja usio na bughudha wa kukaa pamoja na kufanya yao.

Imesimuliwa kuwa kulikuwa kuna sahaba mmoja ambaye alienda vitani lakini huku nyuma kijana wake mdogo alikuwa hoi taabani anaumwa na baada ya muda alifariki na ikatokea kwamba siku aliyorudi ndio mtoto alifariki, lakini mama yule japo alikuwa na msiba wa mwanaye lakini alijipamba vizuri na kujiweka tayari kwa ajili ya mumewe, alipofika alimkaribisha na kushirikiana naye tendo kwanza baada ya hapo ndipo alimpa taarifa za kifo cha mwanaye. Na tendo hilo liliwapa mtoto wa kiume ambaye alikuja kuwa mtu mwema na mzuri.

Huu ndio mfano naweza kuwaachia chini ya kichwa hiki cha habari.

Kuzoeana

kuzoeana baina ya wanandoa ni jambo zuri, kwa maana ya kila mmoja kumfahamu mwenzake, lakini kuzoeana huku kunaweza kuzalisha dharau hususan tukianza kwa upande wa mwanamke kwa kutojali usafi wake, mavazi anayovaa, chakula anachopika, nidhamu ya nyumba na mpangilio wake kwa ujumla, na mume pia anaweza kukosa stara ya kuongea maneno ambayo yanaweza kutatiza mwenziwe au kutokuwa na uchaguzi wa maneno, au kuanza kuonana ni wa kawaida mmoja kwa mwingine.

Matatizo mengi ndani ya nyumba yanaweza kusababishwa na moja au baadhi ya tabia hizo, ambazo huenda ikawa hazitokani na dharau, bali kuzoeana, kwa mfano: siku za utoto wa ndoa mwanamke huwa anajali sana usafi wa mwili wake, umaridadi wa nguo anazovaa, usafi wa nyumba na nidhamu ya hali ya juu, upishi wa chakula unaozingatia vionjo na ubunifu, mapokezi yenye bashasha na wakati mwingine hata kumkumbatia mumewe arudipo kutoka kazini. Lakini baada ya kuzoeana yote hayo hubadilika, mwanamke au mwanaume huanza kuhisi kuwa hana jipya la kumuonyesha mumewe au mkewe, hujiona wameshakuwa watu wazima sasa, na mara nyingi utakuta mwanamke huyu anashinda na sare moja kuanzia asubuhi hadi anapopanda kitandani usiku, mambo ya Hinna, nguo za fashion, salon, manukato, kujipamba kwa piko na dhahabu huyafanya pale anapotoka kwenda harusini na sio nyumbani tena. Huku ndio kuzoeana, na tafsiri sahihi ni kudharau.

Lakini watu inabidi tutambue kuwa ndoa ni maisha yote hivyo inabidi kuwa wabunifu kwa wenzi wetu na pia mwenzi wako inabidi ujue ni baraka kutoka kwa Mungu na inabidi iuonyeshe baraka kuwa unaihitaji na kuikadiri.

Mazungumzo

Mazungumzo ni njia muhimu ya kujenga ndoa na kuiimarisha, aidha ni njia ya mkato ya kusababisha kuchokana na kuchukiana. Mwenzi ambaye hajui wakati gani aseme nini na wakati gani asiseme, hujikuta katika wakati mgumu ndani ya ndoa yake. Kwa mfano: Mwanamke ambaye kila anapoongea na mume wake huanza mazungumzo yake kwa matatizo na lawama humfanya mumewe awe na woga kila anaposikia sauti yake, na kuiona nyumba chungu, kwa sababu hakuna binadamu anayependa kusikia matatizo tu wakati wote. Mwanamke wa aina hii huwa anamsubiri mumewe kwa hamu kubwa, na anapofika tu na kabla hata ya kupata rizki, anaanza kumsomea orodha ya matatizo; watoto wamerudishwa shule, karo haijalipwa, shangazi yako amepiga simu mjomba kalazwa Hospitali na kadhalika na kadhalika. Nyumba ya aina hii huzeeka haraka na wanandoa kuchokana. Na mume ambaye huongea na mkewe kwa ukali na shutuma na kuonyesha kuwa ana mapungufu fulani katika utendaji, au anakuwa kama mkaguzi wa kwanini hiki kipo vile kile kipo hivi, mume huyo ana asilimia nyingi za kukosa mvuto mbele ya mkewe.

Na pia ni muhimu kuchagua mafungu ya maneno kabla ya kuyatamka na kujua ni sehemu gani utumie maneno gani, kuna maneno ya faragha na maneno nje na kwa wapenzi hasa wana ndoa ni lazima wajue kutumia lugha rahisi na tamu miongoni mwao, kwani neno ulitamkapo halirudi tena kinywani na athari ya neno huchoma zaidi ya mkuki na hudumu kwa muda mrefu akilini hata kama kwa dhahiri mtu ataamua kujisahaulisha.

Maneno kama hukua chaguo langu, huniridhishi au hunijali, huthamini hisia zangu ni maneno ambayo huondoa hata hamu ya tendo lenyewe la ndoa. Kuna mfalme mmoja aliongea maneno fulani yaliyo wakwaza wafuasi wake, moto ukaanza kuwaka mitaani wakimuongelea mfalme huyo mwenye maneno machafu asiye na hekima kabsa, Mfalme alifikiri na kujaribu kutafuta njia, ni namna gani atayarudisha nyuma maneno yake, alipata wazo la kwenda kwa Mzee mmoja aliyejulikana kuwa na hekima sana, baada ya kumuelezea yanayomsibu Mzee alimuomba aende nyumbani na kumletea gunia la sufi, Mfalme alipokuja nalo Mzee yule alimuamuru tena kwenda kulifungua katika mtaa na kuacha sufi zisambae, Mfalme baada ya kutekeleza na kurudi, Mzee alimuambia kwamba nenda kakusanye zile sufi uniletee tuimalize shughuli yako kabisa na watu wasahau, Mfalme alipandwa na jazba na kumueleza Mzee yule kwamba hilo ni jambo lisilo wezekana kwani sufi zimeshaenda mbali sana na upepo na kutapakaa na siwezi kuzikamata tena moja moja na kuzirudisha, Mzee akamuambia Mfalme yule kuwa huo ndio uhakika wa maneno

Itaendelea. Inshallah toleo lijalo

Hadhi na Utukufu wa Kurani Tukufu

Kutoka Uk wa 1...

Mtukufu (saw)). Qur'ani Tukufu ni hakimu wa mwisho, sio Hadithi. Kwa hivyo, Qur'ani Tukufu inatangulizwa juu ya Hadithi, hata hivyo Hadithi ni muhimu katika kupata ufahamu zaidi wa Qur'ani Tukufu.

Qur'ani Tukufu ni Kitabu cha Kipekee katika Ufasaha na Usemi:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu umahiri na uzuri wa maneno ya Qur'ani Tukufu. Uzuri huu umefikia kiwango ambacho hata wataalamu mahiri wa lugha ya Kiarabu hawakuweza kuleta hata mstari ambao ungeweza kulinganishwa na umahiri na uzuri wa Qur'ani Tukufu. Kwa hakika, tangu Qur'ani Tukufu ilipoteremshwa, changamoto hii imewasilishwa duniani kote kwamba walete kitu kinachoweza hata kulinganishwa na Qur'ani Tukufu, lakini tangu wakati huo, hakuna aliyeweza kuwasilisha chochote kinacholingana nayo kwa kiwango chochote kile.

Hudhur (atba) alimnukuu zaidi Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba utaratibu ambao Qur'ani Tukufu imeteremshwa nao, mpangilio wa mada na Aya zake ni mkamilifu kabisa na ni utaratibu usioweza kuigwa na unawezesha ufahamu wa kweli na kamili wa maana na hakika za Qur'ani Tukufu. Hakuna andiko lingine lenye mchanganyiko wa kimwujiza ya ujuzi, ukweli na hekima. Qur'ani Tukufu inang'aa kama jua na inajiwekea nguvu tofauti kutoka kila jeha. Basi huu ndio uthibitisho wa wazi kwamba maneno haya yanatoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu mchanganyiko huo hauwezi kukamilishwa na mwanadamu yeyote.

Miujiza ya Qur'ani Tukufu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliendelea kumnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba muujiza wa Qur'ani Tukufu ni mafundisho yenye heshima ya khulka njema, kanuni za jamii na umahiri wake, zisizoweza kuigwa. Vile vile ni miujiza inayohusiana na mambo ya ghaibu na bishara zilizotolewa ndani yake. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Ameonyesha dalili zake kwa uwazi kwa namna ambayo huondoa uwezekano wowote wa shaka.

Hudhur (atba) aliendelea kumnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba baraka zilizoonyeshwa katika zama zake zote zilikuwa ni matokeo ya miujiza ya Mtume Mtukufu (saw) na kwa mujibu wa bishara za Qur'ani Tukufu. Leo, wafuasi wa dini nyingine hawawezi kudai kuwa wana miujiza kama miujiza yetu inayotokana na Qur'ani Tukufu. Hivyo, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba miujiza iliyoonyeshwa kwa mkono wake pia ilikuwa ni matokeo ya Qur'ani Tukufu. Ustadi wa Qur'ani Tukufu haukomei kwenye kufuata maneno tu ya Qur'ani Tukufu, bali kama vile utaratibu wa Qur'ani Tukufu umefanywa kwa namna bora, pia unawasilisha mafundisho bora na kamilifu. Mwenyezi Mungu Anasema katika Qur'ani Tukufu:

"(Ni) Mtume aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu anayewasomea sahifa zenye kutakasika. Ndani yake yamo mafundisho ya kudumu."

(Surah Al-Bayyinah 98: 3 – 4)

Hivyo basi, mtu anayesoma Qur'ani Tukufu haoni ila ukweli na hakika ndani yake. Mwujiza wa mabadiliko uliotokea Uarabuni haujafichwa kwa mtu yeyote. Katika kipindi cha miaka 30, taifa zima lilibadilishwa kabisa.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba kama mtu akiitazama tu Surah al-Ikhlas (Sura ya 112), ataona jinsi Mwenyezi Mungu kwa ufupi lakini kwa undani zaidi Alivyoeleza imani ya Umoja wa Mwenyezi Mungu. Kisha kuna Sura al-Fatiha (sura ya kwanza ya Qur'ani Tukufu) inayojumuisha ndani yake muhtasari wa somo zima la Qur'ani Tukufu.

Hudhur (atba) alisema kwamba haya ni mambo yasiyoweza kukanushwa na yeyote. Hudhur (atba) alisema kwamba yeye mwenyewe mara nyingi ameona kwamba wakati jambo fulani linapofafanuliwa kutokana na nuru ya Qur'ani Tukufu katika mkutano wa wasiokuwa Waislamu, wanayathamini mafundisho na kwa hakika wanakubaliana nayo.

Hudhur (atba) aliendelea kumnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba hakuna mantiki rahisi zaidi kuliko ile iliyotolewa ndani ya Qur'ani Tukufu. Mtu anapaswa kuitafakari kwa makini Qur'ani Tukufu, atekeleze yale yaliyoamrishwa na kuacha yale yaliyoharamishwa, na hivyo wanaweza kumridhisha Mungu; hivyo ndivyo ilivyo rahisi kumpendeza Mungu. Utata unaotolewa na wanafikra na wahenga umefanya mambo kuwa magumu na kusababisha watu kuyumba.

Njia za Kumtambua Mwenyezi Mungu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba Qur'ani Tukufu humwezesha mtu kumtambua Mungu Mmoja, wa Kweli. Waaminio wanapaswa kutoa shukrani, kwa kuwa wamepewa Kitabu kinachowafahamisha sifa zote za Mwenyezi Mungu.

Hudhur (atba) alisema kwamba ataendelea kuzungumza juu ya hadhi ya juu na uzuri wa Qur'ani Tukufu katika siku zijazo. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kuelewa mambo haya na kutekeleza mafundisho ya Qur'ani Tukufu.

Sala Ya Jeneza:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba atasalisha sala ya jeneza ya baadhi ya wanajumuiya waliofariki, akiwemo shahidi kutoka Bangladesh. Hudhur (atba) alisema kwamba hivi majuzi wakati wa Jalsa Salana (Mkutano wa Mwaka) nchini Bangladesh, Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya walishambulia mahali pa Mkutano huo, licha ya kutoa uhakikisho wa usalama kutoka kwa serekali ya mitaa. Wakati shambulio hilo lilipotokea, serekali ilichelewa kutoa majibu. Ilikuwa katika mashambulio haya ambapo kijana wetu mmoja aliuawa kishahidi.

Bw. Zahid Hassan:

Zahid Hassan aliyekuwa mtoto wa Bw. Abu Bakr Siddiq wa Bangladesh. Bw. Zahid Hassan aliuawa shahidi wakati alipokuwa akifanya ulinzi kwenye lango la eneo hilo. Alikuwa na umri wa miaka 25. Alikubali Ahmadiyyat mwaka 2019, miezi 3 baada ya hapo aliwasilisha ombi lake la Wasiyyat. Baada ya kuikubali Ahmadiyyah, mara kwa mara alikuwa akimwandikia barua Hadhrat Khalifatul Masih (atba). Ilikuwa ni wakati wa masomo yake ambapo rafiki yake Mwahmadiyya alimwambia kuhusu Ahmadiyyat na baada ya miaka miwili ya majadiliano, Bw. Zahid Hassan aliikubali Ahmadiyyat. Wakati wa shambulio hilo, watu hao walishambulia kwa mawe na aina mbalimbali za silaha, sambamba na kuwasha moto njiani. Wakati wale washupavu walipojipenyeza ndani ya ukuta, vijana Waahmadiyya waliamrishwa kulinda majengo hayo. Katika pambano hilo, Bw. Zahid Hassan alitenganishwa na wengine aliokuwa nao, jambo ambalo washambulizi walichukua kama fursa na kumshambulia kinyama bila huruma yoyote ile. Walimuua kwa ukali sana kiasi hiki kwamba waliweza kumtambua baada ya masaa mawili.

Hudhur (atba) alisema kwamba hii ndiyo hali ya Waislamu wanaoendeleza uhalifu huo wa kutisha. Mtume Mtukufu (saw) aliagiza dhidi ya kuikata miili hata ya maadui, lakini hivi ndivyo wanavyomtendea Mwislamu. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awachukulie hatua washambulizi. Mazishi yake yalifanyika asubuhi iliyofuata. Alikuwa mkarimu sana, hata hivyo kabla ya kuikubali Ahmadiyyat hakuwa na mwelekeo wa kusali. Hili lilibadilika baada ya kuwa Mwahmadiyya, pale alipokuwa haachi kusali. Hakuwahi kusikika akiongea kwa sauti ya juu na mtu yeyote. Alikuwa mwanachama mwenye jazba wa Khuddamul Ahmadiyya na amekuwa akihudumu kama mwenye ofisi. Siku zote alitekeleza majukumu yake kwa uangalifu na umakini mkubwa. Alijitahidi sana kupata elimu ya dini. Barua ya mwisho aliyomwandikia Hudhur (atba) alipokuwa kwenye gari moshi kuelekea kwenye mkutano huo pia alieleza kuwa kulikuwa na hatari mbalimbali, hata hivyo alionyesha uthabiti wake katika imani. Alipoulizwa kwa nini alituma maombi ya Wasiyyat upesi hivyo, alisema kwamba kila kitu alichokisema Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) kilikuwa kweli, na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliamuru kujiunga na Wasiyyat, ndiyo maana alifanya hivyo. Alikuwa mwana wa pekee wa wazazi wake, pia ana dada wawili. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awape subira familia yake, na pia Anyanyue cheo chake mbinguni.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kulingana na ahadi ya Mwenyezi Mungu, shahidi huyu amepata uzima wa milele. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awakamate wahalifu. Watu hawa wanafikiri kwamba kwa kutushambulia wanaweza kukandamiza azimio letu. Hata hivyo, Hudhur (atba) alisema kwamba amepokea barua kutoka kwa vijana wengine nchini Bangladesh waliosema kwamba ikiwa mashahidi zaidi watahitajika basi wako tayari. Kwa hivyo wapinzani hawawezi kufanya chochote. Hudhur (atba) aliwahimiza wanajumuiya kufanya maombi zaidi.

Bw. Kamal Bhada:

Bw. Kamal Bhada wa Algeria aliyefariki tarehe 2 Februari. Alikuwa mwaminio wa kweli na Mwahmadiya mwaminifu. Aliweka nyumba yake wazi kwa Jumuiya kufanya mikutano yake. Ameacha mke, wana wawili na binti mmoja. Licha ya kupewa shida na majirani zake, kila mara aliweka nyumba yake wazi ili watu waitumie kwa sala. Alisema kwamba wataandika historia kutokana na matatizo yanayokabili jumuiya ya Algeria. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba sasa amekuwa sehemu ya historia hiyo. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Amjaalie maghfirah na rehema.

Dk. Shamim Malik:

Dk. Shamim Malik, mke wa Bw. Maqsood Ahmad Malik aliyeuawa shahidi mwaka wa 2010 huko Lahore. Muda fulani baada ya kifo cha kishahidi cha mume wake alihamia Kanada ambako aliaga dunia. Alipata PhD yake, alifundisha katika chuo kikuu na akawa mkuu wa idara, lakini wakati huo huo alisimamia nyumba yake kwa njia bora pia. Aliwahudumia maskini na daima alikuwa na uamuzi mzuri. Alibashiri ujumbe wa Ahmadiyyat kwa jamaa wasiokuwa Waahmadiyya na daima alikuwa akisoma vitabu vya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as). Kitabu kiliandikwa kumhusu yeye kutoka Chuo Kikuu cha Punjab katika uhai wake, ingawa hii kwa kawaida hufanywa baada ya mtu kufariki dunia. Alikuwa haachi kusali. Ameacha mtoto mmoja wa kiume na wa kike wanne. Hudhur (atba) alimwomba Mwenyezi Mungu Amjaalie maghfira na rehema na daima Awaweke kizazi chake imara juu ya imani.

Bw. Farhad Ahmad:

Bw. Farhad Ahmad, mwana wa Bw. Shahab Ahmad Amini wa Ujerumani. Aliaga dunia akiwa na umri wa miaka 26. Alikuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Frankfurt na pia alikuwa katika Waqf-e-Nau. Alitumikia shirika la Khuddamul Ahmadiyya katika nyadhifa mbalimbali. Siku zote alikuwa tayari kutumikia katika cheo chochote alichohitajiwa. Alikuwa akitoka kwenye nyumba ya misheni alipougua. Baadaye ilikuja kujulikana kuwa alipata mshtuko mkali wa moyo. Alikuwa mtoto pekee wa wazazi wake. Hudhur (atba) alimwomba Mwenyezi Mungu awape subira wazazi wake, Amjaalie maghfira na rehema na Anyanyue daraja yake.

Bw. Chaudhary Javaid Ahmad Bismil:

Bw. Chaudhary Javaid Ahmad Bismil wa Kanada aliyeaga dunia hivi majuzi baada ya kuugua kwa muda mrefu. Alihudumu kwa muda mrefu kama msimamizi wa ofisi ya Tehrik-e-Jadid, kwa takriban miaka 25. Pia alihudumu katika nyadhifa mbalimbali akiwemo Amir wa wilaya yake. Ameacha mke, wana wanne na binti wawili. Alikuwa na sifa nyingi nzuri na hasa alipenda Khilafat. Aliwahudumia maskini. Alikuwa mkarimu sana na pia jasiri sana, hata katika hali ya upinzani na mashambulizi. Alitumikia bila kuchoka na alikuwa na imani kubwa juu ya Mwenyezi Mungu. Ugonjwa wake wa mwisho ulikuwa mrefu sana lakini aliuvumilia kwa subira. Madaktari walisema hawajawahi kuona mgonjwa mwenye subira kama huyu. Daima aliomba kwa ajili ya Hadhrat Khalifatul Masih (atba) kabla ya mtu mwingine yeyote. Alikuwa mwalimu bora na baba mkarimu. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba yeye binafsi alimjua yeye vile vile na kwa hakika alikuwa na sifa hizi zote kuu. Hudhur (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Amjaalie msamaha na rehema.

Muhtasari uliotayarishwa na Review of Religions.

...Mwisho

Ahmadiyya Mpigania Uhuru

Na. Mahmood Hamsini Mubiru.

Wapo Wanahistoria wanaoamini kwamba kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika ulikuwa ni mteremko wa Saranda. Hoja zao zimejikita katika Historia ya kisiasa ya Nchi hii. Baada ya vita ya kwanza ya Dunia ambayo wanayoita ya Dunia 1914-1918 makoloni yote ya Ujerumani walipewa wakoloni wengine, ili watawale kwa niaba ya Umoja wa Mataifa wakati huo, League of Nations. Hivyo Waingereza wakaipata Tanganyika na wakaambiwa waifanyishe kazi ili ipate Uhuru wake. Tanganyika haikuwa na walowezi wengi ambao wasingekubali kutoka kirahisi kama walivyokataa kutoka Algeria, Kenya, Zimbabwe, Afrika ya kusini, Ukosekanaji wa kabila moja lenye wingi wa watu na hivyo kujiona bora na haki kutawala wengine. Dini kuu mbili Islam na Kristo zikiishi kwa amani na Lugha ya Kiswahili ambayo inazungumzwa na watu wote. Ingawaje hoja hizi zinachembechembe za ukweli, hata hivyo Historia inatoa Ushahidi kuwa hakuna hata siku moja mtawala hutoa uhuru kwenye sahaniya dhahabu. Uhuru haupatikani isipokuwa kwa kupitia kumiminika Jasho na ikibidi Damu. Tanzania haiwezi kukwe mkondo. Waingereza ni mabingwa wa vitimbwi, husuda, mbinu na ulaghai. Ni wabobezi katika fitina kama anavyo sema ***Shahespeare Katiki Macbeth, Uzuri wa Ua. juu kumbe chini kuna Nyoka***, Waingereza toka Mwaka 1949 hadi 1958, waliendeleza hali ya kucheleweshaUhuru na tayari walikuwa na fikra kuikabidhi Nchi kwa walowezi kama walivyo jaribu na kushindwa huko Southern Rhodesia. Hivi sasa Zimbabwe. Imani yao ni kwamba hatukuwa na uwezo wa kujitawala mwenyewe. Afrika Mashariki, Tanganyikia, Zanzibar, Uganda na Kenya zote zilikuwa chini ya Mwingereza Mara kwa mara Magavana wa Nchi hizi. Walikutana na kukubaliana juu ya Sera ya kuziongoza Nchi hizi. Mfumo walioutengeneza ni kuwafanya watu weupe wachache watwae madaraka na wapewe hadhi ya upendeleo kuliko wengine katika Nchi. Wazalendo walishitakia mwenendo huu na kupambana. Ni mapambano yaliyoepusha TANGANYIKA isitumbukie katika machafuko kama yale yaliyotokea Zimbabwe au Kenya katika kupata Uhuru Nchi hizi zililazimika kutumia mtutu wa bunduki kupata uhuru. Tatizo kubwa la magavana wa Afrika Mashariki ni kufikiria walikuwa wanafahamu vizuri matatizo ya Wananchi kuliko wananchi wenyewe. Kwa kutumia Watemi walidhani wangeliweza kutawala bila shida yoyote. Wazo la kuwa na mabaraza ya



Mtemi Mohammed Kalufya

wawakilishi walio chaguliwa na wananchi lilipingwa vikali na Sir Philip Mitchell ambaye Tarehe 25/02/1947 akiwakilisha sauti ya Magavana wenzie, alionesha dharau kubwa kwa Waafrika. Yeye alisema Waafrika hawajui maendeleo wala ustaraabu. Hivyo wanatakiwa kutawaliwa kwa miaka, angalau watapata Mwanga kidogo. Msomi Mwafrika alimlinganisha na wanafunzi wa Miaka 14. Mwingereza, kwa kumaliza upuuzi wake huo alisema, hawa watu hawana Historia, wala utamaduni wanahitaji kuelimmishwa kwa miaka mingi. Kufuatia makubaliano hayo ndoto ya kujitawala kwa Tanganyika iko mbali wala isisikilizwe, Gavana Edwad Twinning aliweza kubuni wazo la kuwa na Mabaraza ya uwakilishi yaliyochaguliwa na watu. Yeye akawekea mkazo Mabaraza ya kienyeji baada ya yale yaliyochaguliwa na watu. Katika kila Wilaya Watemi wale walichaguliwa na Watemi ndio walioendesha Mabaraza hayo ya tawala za kienyeji. Mabaraza hayo yalikuwa na vibaraka wale waliosema ndio Bwana kwa wakoloni. Hivyo Waafrika walipoamka na kudai haki zao Mabaraza haya kuwasikiliza bali waliwaita wachochezi na wanaotaka kuleta vurugu. Lugha hii inaonesha ni ya siku nyingi katika hali hii ya kutosikilizwa sauti zao, Wananchi wakaona umuhimu wa kuanzisha chombo kinachoeleza matatizo yao TANU ilitumika kwa ubunifu mkubwa nafasi hiyo na kupata wanachama Wakoloni walifurahi kuona kazi nzuri iliyokuwa inafanywana watemi ambao walikuwa na heshima ya kiroho na kisiasa, kuwatuliza Wananchi kutii Serikali .Kutokana na kilio hicho cha watu na kwa sababu yeye alikuwa Mtemi wa watu, katika mazingira hayo hatarishi. Yakuvua heshima yake na Pato Mpigania Uhuru. Mtemi Mohamedi Kalufya alifika njia panda. ***Kuendelea kuwa na Wakoloni kwa kufurahia makombo au kuwa upande wa watu kupigania haki zao.*** Mtemi Mohamedi Kalufya alikwenda upande wa Nchi akajiunga na Chama cha TANU ambacho alikitetea kwa hali na mali hadi ulipopatikana Uhuru Tarehe 09/12/1961. Mtemi Muhamedi kalufya aliendelea kuwa na juhudi za Chama halisia katika ukombozi wa kweli wa Mtanzania hadi pumzi yake ya mwisho Tarehe 05/12/1982. Sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.

Kaa wanasema Waswahili kujikaanga kwa Mafuta yake Serikali ya kikoloni katika miaka ya 40na 50 ilichukuwa hatua za maksudi ili kukidhi mahitaji ya wakoloni huko kwao na hii hasa ndio maana ya Ukoloni.

Hatua hizi *zliwaudhi* wenyeji na Chama cha TANU kikazitumia kama Karata ya Turufu katika kujijengea uhalali wa Kisiasa. Ili kupata malighafi, ''Hatua kadhaa za kilimo zilichukuliwa ili kuongeza Mazao. Wananchi hawakuelimishwa juu ya Sheria hizo na hatua hizo. Kile walichoona wataalam waliona ni halali kwa Wananchi wote kukifata na kukitekeleza, ***Ulimaji wa mazao ya chakula, biashara namna ya kuzuia Nzige, Uzuiaji wa Mmomonyoko wa Udongo,Ujengaji wa majoshi ya N'ngombe, Kuhifadhi Misitu, Kulinda vyanzo vya Maji.*** Siku kumi za kufanya kazi bila malipo. Kwasababu ya kutoshirikishwa katika maamuzi hayo wananchi hawakuwa na mwamko. Walijionea shida kutembea maili kumi kwenda kutumbukiza Ng'ombe katika majosho. Walioshiriki katika maamuzi hayo ni Watemi na vibaraka na wale waliowateua. Hatua hizi zilijenga hasara na uhasama baina ya Wananchi dhidi ya Serikali ya kikoloni na vibaraka wao. Hapo ndipo tunapoona ushujaa na Moyo wa kizalendo wa Mtemi Muhamedi Kalubya alikuwa ameathiriwa na mafunzo ya Islam yanayotaka kushauriana - Mtukufu Mtume Muhammad saw alikuwa na utamaduni wakuomba na kupokea Ushauri. Kiburi hiki cha Serikali ya kikoloni kutowashirikisha watu katika uamuzi kulijenga hasira na hivyo kujiunga na TANU ili kukomesha kiburi hicho. Na furaha yao ya kujiunga na TANU iliongezeka kwa sababu nyuma yao alikuwa kiongozi wao Mtemi Mohamed Kalufya ambaye alikuwa wa kwanza kuchukua kadi ya TANU. Wakati TANU ikiendelea kuteka nyoyo za Wananchi Wakoloni hawakulala. Walikuwa wakitengeneza mbinu za kuhakikisha kuwa mamlaka na madaraka vinaendelea kuwa katika Mkono ya Wazungu Wahindi licha ya ukweli ya kwamba Waafrika ndio wengi jambo lina heri na shari zake. Juhudi zao hizi za kudharau waafrika kuwa hawawezi ni watu Duni zilijenga na kuamsha kuupenda na kuuthamini Uafrika. Kama walivyofanya watu Weusi Nchini Marekani, Wananchi wakapita wakinadi uweusi wao na kusema kuwa Weusi haikuwa alama ya matusi bali ni neema ya Allah. Yaliyokuwa yanatokea Ghana chini ya Kwame Nkurumah ya kupigania heshima ya watu Weusi yakazidi kuwatia watu moyo. Maneno ya Kwaguyir Aggrey ambaye katika miaka ya kabla alitembelea Tanganyika yalieleza kila mara ''***Mimi ni mweusi Nikifa nikaambiwa kurudi ningependa kurudi na rangi gani nitasema nifanye mweusi kuliko nilivyo kwa hivi sasa.*** Wale wote walione Fahari na sio kinyaa kuwa Waafrika

Itaendelea. Inshallah toleo lijalo

Bustani ya Washairi

Binti Mwanafunzi:

Nakupatia madini, kwa wazi bila kusita
Akili isiwe duni, badae uje kujuta
Jipambanue kichwani, mbeleni usije sota
Salama yako elimu, mapenzi utayakuta.

Unapokua shuleni, na kukalia kibweta
Achana mawazo duni, ni lini utampata
Acha kuwaza ukuni, na mimba hutaipata
Salama yako elimu, Mapenzi yatakuzika

Usije sema ya nini, elimu ya komputa
Kumbuka upo shuleni, usipende kutakata
‹Tatamanisha wahuni, na kitambi utapata
Salama yako elimu, mimba usijibebeshe.

Matiti yako mwilini, yanakupa uzuzuta
Na ngozi pia laini, mazombi inawavuta
Umbo dogo la tumboni, mamende wanatepeta
Salama yako elimu, soma sana we mtoto

Sina kona wala nini, watoto mna matata
Mara wazi kifuani, nini mnakitafuta?
Au aseme kuhani, kichwani vitakamata?
Salama yako elimu, usichana unapita.

Mwafunzi uko shule, kazi yako ni kusoma
Acha kupiga kelele, kutwa unasema sema
Ukishafeli ndo vile, nimekumbusha mapema
Salama yako elimu, soma sana we mtoto.

Kichwanimo mko tele, miluzi inarindima
Mara Ally mara Sele, nyota wataka izima
Tuliza hicho Kipele, ‘sifuatishe mtima.
Mapenzi mwana ukome, yataizimisha ndoto.

Achana makundi yale, wanakupotosha Mama
Wanapenda vya bwelele, wataja kufa na ngoma
Iweke elimu mbele, muone Samia Mama
Mwanaume Baba yako, wengine wote Majoka.

Sipende kula mchele, utakusumbua Mama
Wewe kazi yako shule, unaitwa wa kusoma
Mchele huu mchele, uelewe naposema
Salama yako elimu, mchele unalegeza.

Nakusihi Tumpale, mzazi anakupima
Embu kazania shule, cheza pia ila soma
Tafakari waza mbele, usichoke kujituma
Urembo wako si kitu, pata sifuri uone.

Binti tulia tuli, ngono acha Mwanamboka
Ni kweli bado kimwali, na mashavu yanawaka
Mapenzi usiwe nguli, usipende kujipoka
Raha ya kuwa mrembo, kichwani muwe na kitu.

Urembo bila akili, Mwili utakongoroka
Usikomaze akili, mapenzi kuyakumbuka
Soma utulie tuli, mbeleni utarembuka
Sasa wajiona mwali, uso haujababuka

Wapige chenga ya mwili, usiwaze kungonoka
Mapenzi kwako batili, subira yahitajika
Usijipige utuli, mamende yatavutika
Raha ya kuwa mrembo, kichwani muwe na kitu.

Kifuani saa sita, usiringe kaa mbali
Vijana watayavuta, yawe kama santuli
Dunia uwanja tata, jisitiri na kufuli
Hayawani hana jema, king’ang’anizi hatari.

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Kalindimasenior@gmail.com

DUNIA YAFURA

Dunia Yafura nzito, Rohoye yapata joto
Ukame ikavu mito, Nafsi zakana wito
Tutsi hutu soweto, Damu zajaza mito

Magharika yatuvaa, Ajali zachinja koo
Binadamu hoi njaa, Msululu matukio
Vimbunga tetemo pia, Na hakuna kimbilio

utandawazi jamani, Maasi hadharani
Kheri, dhila vi machoni, Elimu na mitihani
Koo kavu taabani, Hufyonza vya mitaroni

Mbiu hamasa za mwasi, Zapoza silika wema
Shida kupita kiasi, Zaangukiwa na ngema
Misada yawa vifusi, Pokea inasakama

Hino dunia papasi, Fikira na macho pofu
Wamezagaa khanasi, Wapotoshi uongofu
Jefule chanzo mikosi, Ikimbizayo minofu

Nafsi zawa katili, Na maamuzi hamaki
Nuru yavikwa kivuli, Akili zataharuki
Na hana shauri mbili, Mja kurusha mkuki

Haitufunzi elimu, Ya uzoefu chukua
Haziogofyi hatamu, Zinoghubika dunia
Vifo vya wa rika tamu, Vitukinahi dunia

Haitaongoka roho, Bila tambua Molake
Haitatulia roho, Bila kizingiti chake
Akili hafidi joho, Bali ni kwa nuru yake

Mtafute kwa juhudi, Piteni kwa wake Waja
Ziweke vyema kusudi, Na useme Mola naja
Naye latifu hamidi, Msikivu wa lahaja

Shunda Mshundia Wana
Daluni – Tanga

Pole Mjadidi

Yametufika mauko, Matozi yatumwaika
Mametu tena hayuko, Hancha kabaki Upeka
Dunia kwetu kivuko, Kivuko kiso hakika
Pole mjadidi pole, kwa hayo yalo kukuta.

Tumepata msituko, neno lilipotufika
Tunalia ndugu zako, kichwani tumejishika
Hili kweli tikisiko, yakuti imeanguka
Pole mjadidi pole, kwa hayo yalo kukuta.

Dodoma japo hatuko, nyoyo zetu zishafika
Uliko na sisi tuko, nyamaza nyamaza Kaka
Kifo kimekosa mwiko, yoyote kinamteka
Pole mjadidi pole, kwa hayo yalo kukuta.

Kesho ni yake maziko, Mungu atupe baraka
Tumpe mapumziko, mamaetu msifika
Adhabu zilizo huko, muepushie Rabuka
Pole mjadidi pole, kwa hayo yalo kukuta.

Kadi tamati andiko, mikono yutetemeka
Si kwangu wala si kwako, nasi yetu itafika
Nasadiki siku iko, mama tutajumuika
Pole mjadidi pole, kwa hayo yalo kukuta.

Hamis Kisamvu
Dar es Salaam

Pole sana mjadidi, kufa pia ni Rehema
Tungelidama abadi, pasi kufa na kuhama
Tungepata nyingi itadi, kwani Dunia si njema
Sisi ni wake Rabana, nak wake tutarejea.
Mhariri

Bishara imetimia

Siku muhimu ya leo, sawa na historia
Tarehe kama ya leo, bishara kainadia
Mola tampa mzao, dini taitumikia
Bishara imetimia, leo twasherehekea .

Seyyidina ahmadi, aliambiwa na mungu
Mwana aliye mweledi, atapewa jema fungu
Jamati atainadi, china hata kwa wazungu
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Ndani ya miaka tisa, mwenyezi alitamka
Kitakamilika kisa, mwana ataja oneka
Masihi aliwahasa, wahindu wenye haraka
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Leo twasherehekea, bishara kukamilika
Yote yameshatimia, yalonenwa na rabuka
Elimu kaizamia, inashangaza hakika
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Jamati kaieneza, ulaya na afirika
Kila aliloliwaza, halikukosa Baraka
Mola aliye muweza, kamkuza kwa haraka
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Ni matukio lukuki, mola aloahidia
Kumaliza sidiriki, yote kuyahadithia
Bali naapa kwa haki, bishara imetimia
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Mwl. Mustafa Mambo
Sauti Nyembamba
Likokona Jamaat

Usikatae mitala

Mjenzi ndiye mjuzi, kwakile alokiunda
Aloijenga kurunzi, mbali sana akakwenda
Akiba akamaizi, vifaa akaviunda
Usikatae mitala , mjenzi ndiye mjuzi

Hebu mwangalie kuku, jogoo alokomaa
Matembe wenyeshauku, dhamana humpatia
Waamsha mwanzo siku,namwewe kuwaambia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Muumbaji anajua, ndiyo mana akasema
Rukisa wewe kuoa, wanawake walowema
Moja Hadi nne oa, kuzidisha sio wema
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Akili yako tumia, mitala ukizuia
Wale wanaobakia, utawa watatulia??
Kama hawatatulia, Nini Sasa chafwatia??
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Akili yako tumia, Nini kitachotokea
Usawa tukitumia, mitala kwa mke pia
Mimba mke kipatia, baba yupi atalea
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Kumbuka nakuambia, Kila mwana anababa
Jini wanazichangia, nusu mama nusu baba
Ugomvi utauzua, kugombania ubaba
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi

Hayo Kenda nakwambia, kumi hili lisikia
Siku zikishakujia, au mwana ukazaa
Waume tavumilia??au dhambi tawatia
Usikatae mitala, mjenzi ndiye mjuzi.

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

Mti wa matufaa



Hapo zamani, palikuwa na mti mkubwa wa matufaa. Mvulana mmoja alipenda kwenda na kucheza nao kila siku. Alipanda juu kabisa, alikula matufaa. Alilala kwenye kivuli chake. Aliupenda mti na mti ulipenda kucheza naye.

Muda ukasonga. Mvulana sasa akawa kijana na hakucheza kule mtini tena. Siku moja, kijana alirudi kwenye mti na akagundua kuwa una huzuni.

" N j o o ucheze nami" mti ulionekana kumuomba kijana. "Mimi sio mtoto tena, sichezi kwenye miti," kijana alijibu. "Nataka vikorokoro vya kisasa vya kuchezea. Nahitaji pesa kuvinunua."



"Pole, lakini sina pesa, ila waweza chuma matufaa yangu yote na kuyauza. Ndipo utapata pesa." Kijana alifurahi sana. Alichuma matufaa yote mtini na akaondoka akiwa na bashasha. Kijana hakurudi tena baada ya kuchuma matufaa. Mti ulihuzunika tena.

Siku moja, miaka mingi baadaye, kijana aliyekuwa sasa mwanaume akarudi na mti ukafurahika sana! "Njoo ucheze nami," mti ulionekana kusema. "Sina muda wa kucheza. Inabidi nifanye kazi kwa ajili ya mke wangu na watoto. Tunahitaji nyumba ya kujistiri. Unaweza nisaidia?" mwanaume alijibu.

"Samahani, sina nyumba yoyote. Lakini unaweza kukata matawi yangu kujengea nyumba yako."

Basi mwanaume akakata matawi yote kwa furaha na kuondoka akitabasamu. Mti ulifurahi kumuona tena lakini mwanaume hakurudi tena kwa miaka na miaka. M t i ulikuwa mpweke tena na ukakasirishwa.

Siku moja ya kiangazi, mwanaume alirudi na mti ukafurahi. "Njoo ucheze nami," mti ulisema. "Nakaribia miaka hamsini. Nataka nipige tanga ili niburudike kipindi cha likizo. Unaweza kunipa jahazi?" aliuliza mwanaume.



"Tumia kiwiliwili changu kujengea jahazi lako. Utaweza kupiga tanga mbaali na ukaburudika," mti ulionekana kujibu.
Basi mwanaume akaukata mwili wa mti kwa furaha kutengenezea jahazi. Akaenda kupiga tanga na hakurudi kwa kitambo kirefu.

Hatimaye, mwanaume alirejea baada ya miaka mingi. "Samahani kijana wangu. Lakini sina chochote kwa ajili yako tena. Sina matufaa," mti ulionekana kusema.

"Hakuna tatizo, sina meno tena ya kung'atia," mwanaume alijibu

"Sina mwili wa kunipanda tena," mti ulionekana kujibu.

"Nimezeeka sana kwa hilo sasa," mwanaume alijibu.

"Kweli siwezi kukupa chochote kijana wangu. Kitu pekee nilichobakia nacho ni mizizi yangu inayojifia," mti ulionekana kusema na machozi.

"Sihitaji mengi sasa, sehemu tu ya kujipumzishia. Nimechoka baada ya miaka yote hii," mwanaume alinena.

"Vyema! Mizizi inayojizeekea ndio sehemu nzuri ya kuegema na kupumzika, njoo ukae nami kitako upumzike," mti ulionekana kunong'ona kimoyomoyo.



Mwanaume akakaa kwenye nyasi akiegemeza mwili wake dhaifu kwenye kisiki. Mti ulifarijika sana hata ukaonekana ukitabasamu kwa machozi...

Hadithi hii inatufundisha nini?

Baraka zote ni za Muhammad[saw]



Na. Nasir Bin Khalid.
(Katoma, Kagege - Kagera-TZ)

Bismillahir Rahmanir Rahiim

Katika kuitalii Quran Tukufu kwa makini nikakutana na maneno adhimu katika Sura 91:03 ambayo inasema hivi kwamba nina nukuu ***'Na kwa mwezi unapoliandama'.*** Aya hii imefafanuliwa vyema katika maelezo ya Quran Tukufu ya kwamba Muradi wake ni Masihi aliyeahidiwa[as] au watawa watakao chukua Nuru ya Mtume[saw] na kuizagaza Duniani kote, kama vile mwezi unavyoakisi Nuru ya Jua na kuisambaza tena Duniani wakati wa giza. Hapo ikanipelekea tafakuri yangu kwenda mbali na kuanza kutafakari madhila yanayotokea Duniani.

Nikagota hasa kwenye janga hili la Ushoga na vitendo vichafu vinavyozidi kukithiri. Ndipo nikakumbuka maneno ya Mwenyezi Mungu yanayosema kwamba ***"Hakika kwamba Mwenyezi Mungu hawezi kuleta adhabu bila kutanguliza Muonyaji"*** na maovu haya yanayoashiria kuwa hizi ni zama za ujio wa yule aliyeahidiwa kuja kwani kuhusu zama zake Qurani Tukufu inatueleza kwamba ***"Na Mitume watakapokusanywa"*** hii ikamaanisha zile jumbe za Mitume wote zitahitajika tena katika ujio wake, kwani maovu yale yatakuwa yamerudi tena na kushika kasi.

Hivyo basi muonyaji ameshafika ambaye ndiye suluhisho la matatizo yote na ndiye muafaka wa majibu yanayotafutwa na viongozi wote wa Duniani, Je tusubiri adhabu au tumpokee aliyedai kuwa Masih aliyeahidiwa? ambaye ni Mirza Ghulam Ahmad[as] kwani kumpokea na kumfuata yeye ndio suluhisho pekee.

Na yeye ndiye Mwezi unaoakisi Nuru ya Mtume Muhammad[saw] kama vile Mwenyezi Mungu alivyompasha Habari kwamba "Baraka zote zinatoka kwa Muhammad[saw]".

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 25 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

R	M	M	S	N	G	R	X	D		J	T	L	T	A	H	R	I	K	
T	K	X	A	B	M	V	H	A	Q	N	M	S	I	K	I	T	I		M
Z	F	N	N	D	L	W	B	G		M	A	K	A	L	A		M	K	A
K	Z	V	D	H	P	I	A	A	W	M	Z	K	M	N	J	D	L	J	U
M	M	H	A	X	T	D	N	L	L	T	A	H	K	B	N	Q	N	T	U
T	Y	Y		A	Y	A	M	F	I	Y	T	S	K	F	R		X	Z	D
C	A	Q	K	G	L	Z	Z	L	T	M		N	I	M	A	I	T	I	
Q	S	P	M	U	V	K	X	A	A	A	U		P	H	G	R	G	N	J
X	S	M	A	A	R	B	Y	B	H	H	U		S	P	I	M	Z	K	K
N	A	M	A	J	Z	Y	A	S	R	M	M	A	N		J		M	B	Q
P	R	Q	K	S	I	I	I	R	E	L	R	A	I	L	R	M	W	U	B
W	N	N	L	S	H	M	S	H	A	B	T	N	D	M	W	M	F	K	M
N	A	M	A	C	I	A	E	H	A	B	A	M	V	I	Z	Z	J	H	U
P	L	W	C	S	Z	R	I	K	I	I	A	P	R	X	Y	Y	A	A	O
R		D	A	N	A	Y	D	R	R		Z	R	R	C	M	Y	M	R	N
P	P	R	D	M	N	D	L	U	I	L	L	P	A	R	Z	G	A	I	G
C	R	Z	Z	P	N	T	B	Q	T		Q	T	Z		M	H	A		O
K	F	K	T	M	H	G	K	R	C	N	L	C	N	H	N	T	T	G	Z
T	K	D	F	A	L	S	A	F	A		W	R	M	B	Y	G		L	O
M	W	M	W	G	N	M	T	U	T	A	M	B	U	Z	I		Y	M	

Jinsi ya Kupika Cake za Nazi



VIPIMO

1. Unga ½

2. Kikombe Cha Sukari ½

3. Kikombe Cha mayai ¼

4. Baking powder ½ kijiko cha chai

5. Maziwa kiasi tuu & Tui LA Nazi

6. Vanilla ½ kijiko

NAMNA YA KUPIKA KEKI

1. Tia siagi sukari na baking powder piga kutumia mashine(mchapo) mpaka iwe laini

2.Tia mayai na uendelee kupiga

3. Tia unga polepole huku ukiendelea kuupiga ongeza na tui la nazi

4. Tia maziwa na vanilla piga kidogo tumia treya ya vishimo(muffin tray) weka karatasi zake kisha mwaga ule mchanganyiko katika vishimo kiasi kiasi chunga usivijaze sana

5. Choma(bake) katika moto wa 325°c kwa dakika 10-15 mpaka iwe rangi ya uthurungi(brown)

6. Epua Hapo itakuwa Tayari kuliwa

Jamia Ahmadiyya Morogoro yatoa Zawadi ya Idd-ul-Fitr.

Kutoka Uk wa 1..

mheshimiwa Fatma A. Mwassa.

Hafla ilianza kwa usomaji wa Qurani Tukufu iliyosomwa na Hafidh Abdur-Rahman Ramadhan Rundo na kufuatishwa na utambulisho wa wageni na utambulisho mfupi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa mgeni rasmi na wananchi kwa ujumla, kazi ambayo ilifanywa na Maulana Sheikh Abid Mahmoud Bhatti Sahib aliye ni Naibu Amiir Jamaat na mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya – Tanzania.

Katika utambnulisho wake, Naib Amiir Sahib alieleza kwa muhtasari wasifu na vyeo vya mwanzilishi mtukufu wa jumuiya ya Waislam Waahmadiyya – Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian. Kisha aliishukuru sana na kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sera yake thabiti ya kutoegemea upande wowote katika suala la dini na kuwaacha wananchi kujichagulia dini waipendayo bila ya kubughudhiwa ilimradi wafuate sheria za nchi. Aidha, Naibu Amiir Sahib alieleza kazi mbali mbali zinazofanywa na Jumuiya hii hapa nchini katika nyanja za elimu, afya, maji n.k.

Pia Naib Amiir Sahib aliongeza kwa kusema kuwa Jumuiya hii ikiwa ni ya Kiislamu inayofuata kikamilifu mafundisho ya Mtume Mtukufu (saw), daima inawafundisha wafuasi wake kwa ujumla lile fundisho la Mtume Mtukufu (saw) lisemalo kuwa, "kuipenda nchi (yako) ni sehemu ya Imani." Hivyo wafuasi wa Jumuiya hii daima huipenda nchi, kujali ubinadamu na kuthamini amani, umoja na mshikamano uliopo hapa nchini.

Baada ya utambulisho huo wa Naib Amiir Sahib, zilifuata nasaha fupi za mwakilishi wa mwenye kiti ya mitaa ya kata ya Kihonda Maghorofani na kufuatia nasaha fupi za diwani wa kata ya Kihonda Maghorofani, Mheshimiwa Hamisi Ndwata ambaye katika maelezo yake alimweleza mgeni rasmi ya kuwa anaishukuru na kuipongeza sana Jumuiya hii kwa jinsi inavyochangia shughuli za maendeleo katika kata yake. Amesema kuwa wanajumuiya Waahmadiyya wamekuwa na mwitikio mzuri sana katika kujitolea kifedha na nguvu kazi pia.

Kisha zilifuata nasaha za mgeni rasmi Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, ***Mh. Fatma Abubakar Mwassa***, ambaye baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliishukuru sana Jumuiya pamoja na viongozi wake kwa kuandaa mpango huu maalum wa kuwakumbuka wenye uhitaji. Alisema, mema haya mnayoyafanya hakika hatuna uwezo wa kuwalipeni bali ni Mwenyezi Mungu tu Ndiye Awezaye kuwalipeni. Akizungumzia mchango wa Jamaat katika uwanja wa kielimu, alisema kuwa elimu ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu na ndiyo sababu sura ya kwanza kabisa kushuka imesema, "IQRA'." Alisema elimu pekee ndiyo inayompa mwanadamu maarifa ya kutenda mema na kuacha maovu. Ni elimu pekee itakayomfanya mwanadamu awe na hofu ya Mwenyezi Mungu, na akiwa na hofu ya Mwenyezi Mungu, basi maovu yote yanayosemwa yataisha.

Akizungumzia suala la afya, Mheshimiwa mgeni rasmi alisema kuwa anatambua kuwa Jamaat inayo hospitali nay eye kama sehemu ya serikali watajitahidi kuweka mazingira bora ili Jumuiya iendelee kutoa huduma bora kwa wanchi.

Baada ya hapo zoezi la utoaji wa zawadi likaanza ambapo naye alipatiwa zawadi maalum ya vitabu vya dini ikiwemo pia tafsiri ya Qurani Tukufu. Hafla ilihitimishwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mheshimiwa Naib Amiir. Kisha sala za adhuhuri na alasiri zilisaliwa kwa pamoja. Tukio hili limeripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari kama vile redio, runinga, magazeti na katika mitandao ya kijamii.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[AS]

Kudhihiri kwa Mwenyezi Mungu

Naam, Mweza wa yote na Mwenye nguvu ni yule Mungu Ambaye Waumini Wake hawatahasirika kamwe; wale wamjiao kwa mapenzi na uaminifu. Adui hujigamba kwamba atawaangamiza wote kwa ushetani wake na mwenye nia mbaya huapa kwamba atawamaliza. Wapumbavu ninyi, Asema Mwenyezi Mungu, je, mtajasiri kupigana nami? Na kumdhalilisha yule aliye mpenzi wangu? Kwa hakika, lolote haliwezi kuikumba dunia hii ila liwe limekadiriwa hivyo huko mbinguni, wala hakuna mkono wa kidunia uwezao kufikisha dhoruba zake nje ya eneo ulilopimiwa huko mbinguni. Hivyo basi, wenye kula njama za uovu na ukatili ni wapumbavu mno ambao katika harakati za mipango yao miovu ya aibu, hawamkubali Yule Dhati Mkuu Ambaye hata jani haliruhusiwi kudondoka bila ya amri Yake. Kwa hivyo, wao huibuka na kushindwa na shabaha zao kutotimia; wala njama zao haziwadhuru wale walioongoka; kinyume chake ishara za Mungu huenea zaidi na fahamu za watu juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu huongezeka. Yule Mungu Mweza, Mwenye nguvu, Asiyeonekana kwa macho, Hujidhihirisha kwa hakika kupitia kudra Zake za ajabu.

(Roohani Khazain Jal. 13: uk. 19: Kitab-ul-bariyya, Muqaddama uk. 1)

TANGAZO LA IJTIMAA YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atafal wote nchini kuwa Ijtimaa yao itakuwa tarehe 23 - 25 Juni 2023, Kitonga, Wilaya ya Ilala, Da. es Salaam.

In-Shaa-Allah.

Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuendelea na maandalizi ya Ijtimaa hii na kuichangia pia sawa na matakwa ya katiba.

Usipange kukosa!

Limetolewa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

MATUKIO KATIKA PICHA



Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Bi. Fatma Abubakar Mwassa, akihutubia katika hafla ya ugawaji wa zawadi za Eid-ul-Fitr huko Morogoro, Meza kuu kulia akiwa ni Sheikh Karrimuddin Shamsi Sahib akifuatiwa na Naib Amir Maulana Sheikh Abid Mahmood Buthi



Picha ya pamoja ya Naib Amir na Mkuu wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya, Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhutti Sahib pamoja na Masheikh mara baada ya Sala ya Eid ul Fitr kuswaliwa katika viwanja vya Jamia Morogoro.

Wanajumuiya wa jamia Ahmadiyya waliungana na wanajumuiya wengine wote nchini na duniani kwa ujumla katika sala na sherehe za Eid e Fitri iliyosaliwa siku ya jumamosi ya tarehe 23/04/2023. Sala ilisaliwa katika ukumbi wa chuo Kihonda Morogoro, na iliongozwa na Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib Principal Jamia Ahmadiyya na Naib Amir Jamaat Ahmadiyya nchini Tanzania.

Katika hotuba yake ya sala ya Eid, Naib Amir sahib aliwakumbusha waumini historia ya saumu ya kwanza na sala ya kwanza ya Eid katika dini tukufu ya islam. Aidha aliwakumbusha wanajumuiya namna na njia sahihi ya kusherehekea sikukuu ya Eid, alisema kuwa furaha ya kweli kwa mwislamu ni ile inayoambatana na kutafuta radhi ya Allah na ndio sababu pia ya kuwa siku ya Eid sala huongezeka kutoka sala tano kwa siku na kuwa sala sita. Na katika sala hii ya Eid tunatamka takbira kumi na mbili takribani katika rakaa mbili tu, hii yote inatuonyesha kuwa hii ni siku maalum ya kumtukuza sana Allah na kumsalia sana mtume mtukufu saw. Katika nasaha zake, Naib Amir sahib pia aliwakumbusha wanajumuiya kuzidi kumuombea Hadhrat Khalifatul-Masihi v a.t.b.a ili Allaah Amjaalie afya njema na umri mrefu ili aendelee kuiongoza jamaat yake hii tukufu.

Pia aliwakumbusha wanajumuiya kuendelea kuwaombea ndugu zetu Waahmadiyya wa Pakistan, Al-Jazaair, Bangladesh, Indonesia na Burkinafaso ambao wanateswa na kuuawa kwa sababu ya imani yao.

Mwisho, aliwafikishia wanajumuiya salamu za Eid kutota kwa Amir sahib Maulana Tahir Mahmood Chaudhary na alimaliza hutuba yake kwa maombi ya kimya. Aidha katika kuonyesha mapenzi yake kwa watoto, Naib Amir sahib aliwagawa zawadi mbalimbali ikiwemo pia fedha. Na mwisho wa hafla hiyo wanajumuiya walipata chakula cha pamoja kilichoandaliwa na idara ya Jamia kwa idhini ya Principal sahib.

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka tolro lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 3



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Ndugu wasomaji wapendwa,

Kabla sijaenda mbali zaidi na muendelezo huu wa Makala hizi, napenda niweke bayana namna wanajumuiya ya Mwanza mjini walivyojitolea kimahubiri kwa nafsi zao na mali zao. Wanajumuiya hawa wa Mwanza ndio waliokuwa chachu ya vuguvugu hili la mahubiri ya mkoani Shinyanga, kwani harakati kadhaa zilishaanza na nitazigusia.

Wanajumuiya wa Mwanza wakiongozwa na Rais wa Mkoa (wakati huo) mzee Salim Thani, na msaidizi wake yaani Naib Rais (wakati huo) ndugu Yahya Kambaulaya walifanya juhudi kubwa na uratibu mzuri sana wa mashauriano namna ya kufanya mahubiri mkoani Shinyanga. Na kubwa zaidi, hazina ya wazee (kushauri) ikatusaidia sana namna ya kuyaendea mahubiri hayo.

Na kwa kupitia mashauriano hayo mema, ikaanzishwa desturi ya kila Ijumaa mara baada ya sala pale msikitini Nyegezi stand (msikiti mdogo wa zamani) wanajamaat waketi kwa muda na kushauriana. Wanajamaat wa Mwanza wakaitikia wito wa viongozi wao na kuanza kushirikiana kikamilifu kuhusu kushiriki mahubiri Shinyanga. Ambapo mashauriano hayo yakapokelewa vema sana, huku wajumbe wengi wa Majlis ya Mkoa wakikiri kuwa hii ni fursa kwa Jamaat ambayo Allah ametuletea, tuikazanie na kuisimamia.

Na kweli tukaanza kuikazania kusimamia.IkashauriwakilaJumamosi na Jumapili basi wanajumuiya watoke Mwanza na kwenda Shinyanga vijijini kufanya mahubiri, na wale wanaoweza kujitolea kukaa huko kwa siku kadhaa basi na wafanye hivyo. Nakumbuka wazee wetu waliingiwa na jazba nzuri sana kutuhamasisha sisi Khuddam wakati huo, huku wazee hao wakitutolea mifano mingi ya mahubiri waliyokumbana nayo tangu miaka ya sitini na sabini huko. Nakumbuka michango ya hamasa kutoka kwa mzee Mwl Omar Matimbwa sahib, mzee Saidi Sasamka sahib, marehemu mzee Kelebuse sahib na wengineo. Huku Khuddam nao hawakuwa mbali kwenye joto la kuongeza nguvu ya mahubiri mkoani Shinyanga wakiongozwa na ndugu Yahya Kambaulaya sahib, bwn Yusuf Kachima sahib, Mwl Ramadhan Mahmood sahib, ndugu Ahmad Thani sahib na wengineo kadhaa.

Wakati huo pale Shinyanga alikuwa ameshapelekwa mwalimu wa kwanza kusimamia shughuli za Kijamaat na alikuwepo Mwl Twaliat Zuberi sahib, na kusaidiana nae mahubiri vijiji vya Negezi, Bugimbagu, Mwawaza na maeneo ya Shinyanga mjini. Pale Shinyanga mjini ilikuwa ni chimbuko pia la familia yam zee Salim Thani, na pia kulikuwepo na wanajamaat vijana waliohamia kutoka mkoani Tabora wakifanya shughuli zao Shinyanga mjini akiwemo bwn Baraka na mtoto wa mzee Ngayabula wa Mwanza. Wote walishirikishwa kikamilifu.

Basi ikawa kila ijumaa pale jijini Mwanza tunachanga senti kuwezesha mahubiri, mwenye kiasi chochote aliruhusiwa kuchanga ili kuwezesha mahubiri na malezi ya mwanzo kabisa huko Shinyanga. Na kwa kiasi kikubwa kabisa nikiri kuwa, sehemu kubwa ya mchango kuwezesha mahubiri yale na kambi vyote kwa pamoja ilidhaminiwa na ndugu Yahya Kambaulaya kwa kujitolea kwake. Hakika hii ilikuwa ni jihadi kubwa ya vitendo, wengi tulijifunza.

Wanajamaat wa Mwanza ikageuka na kuwa ndio desturi yetu, kwamba kila ifikapo Jumamosi na Jumapili basi tulikuwa tukielekea mkoani Shinyanga. Huko tukajitahidi mahubiri, kufanya malezi, kununua viwanja vya misikiti kwa kujitolea. Na kubwa zaidi ikawa ni wanajumuiya ya Mwanza kuhakikisha kuwa misikiti inajengwa kwa kupitia waqar e amal. Tukawa tunachukua vijana mafundi wa ujenzi kutoka Mwanza akina Kelebuse na wengine kutoka palepale Shinyanga, huku tukiwahimiza mafundi hawa Khuddam waweke kambi kule na kuhakikisha msikiti unajengwa. Japokuwa kulitokea changamoto kadhaa za kiujenzi hususan msikiti wa Bugimbagu, ikipelekea msikiti ule kubomoka mara mbili katika kipindi kifupi cha ujenzi. Tulibaini baadhi ya changamoto zilizojiri, na hatimae tukazitatua vema.

Kwa kuona umuhimu wa tawi lile la Bugimbagu, ikatulazimu kuomba msaada apatikane Daiyan aje kusimamia tawi hilo wakati harakati ujenzi wa msikiti zikifanyika. Na Alhamdulillah tulijaaliwa kumpata Daiyyan mzee Habibu sahib kutoka Morogoro na kuja kusimamia tawi hilo, japo kulikuwa na changamoto za upya wa tawi lakini pia ujenzi ule wa msikiti. Na Alhamdulillah tawi liliimarishwa kupitia mzee Habibu sahib. Ikumbukwe kuwa, harakati zote hizi zilienda sambamba kwa kufuata nidhamu ya Jumuiya kwa kila kitu lazima kwanza tupate muongozo wa kiongozi wetu Amir sahib Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib.

Nakumbuka vema kuwa hali hii ya mahubiri na kujitolea katika njia ya Allah ilimvutia sana Amir sahib, na ikapelekea yeye mwenyewe kushawishika kwa kuona wanajumuiya wenyewe wamejipanga na wanatekeleza shughuli za Jamaat kwa kiwango kikubwa sana. Hapo ikamfanya maulana Amir sahib kuanza kuifatilia kwa ukaribu Jamaat za Mwanza na Shinyanga kwa ujumla wake. Pia tukumbuke kuwa, nyakati hizo Jamaat ya Mwanza ilikuwa inasimamiwa na Mwalimu tu, hapakuwepo Sheikh yeyote kwa nyakati hizo. Na mkoa wa Shinyanga ulikuwa chini ya Mwanza, ambapo Rais wa Mkoa wa Mwanza na Majlis yake waliwajibika moja kwa moja kuuhudumia na kuulea mkoa wa mpya wa Shinyanga ambao ulikuwa na matawi yasiyozidi matatu tu.

Alhamdulillah tukajaaliwa kujenga misikiti miwili ya Negezi na Bugimbagu, huku sehemu kubwa ya ujenzi huo ikichangiwa na wanajumuiya wa mkoa wa Mwanza. Kuna safari mbili nakumbuka nilisafiri kwenye gari moja na wazee wetu mzee Saidi Sasamka na mzee Mwl Omar sahib. Hawa ni wazee wenye umri mkubwa kabisa, lakini ni wazee ambao walikuwa na jazba ya hali ya juu mno kujitolea nafsi zao kwa ajili ya Jamaat. Wazee hawa (licha ya umri kuwatupa) lakini waliniambia, babu twende wote na tutabeba tofali. Tutachota maji, tutasogeza mchanga na kazi nyinginezo. Na kweli hawakulala wala kusimama, tuliwajibika nao waqar e amal pale tawini Bugimbagu ujenzi wa msikiti kutwa nzima, hii kwetu ilikuwa ni chachu kubwa sana kiimani. Nyakati hizo, sisi wengine tulikuwa ni vijana miaka 30 hivi. Kwa hakika, mbiu ya hawa wazee ilituamsha na kutuimarisha san asana.

Kama vile haitoshi, mwaka huo wa 2012 tulifanya kambi kubwa ya kimahubiri kijijini Sungamile. Kambi hii tena ilikuwa chini ya wanajumuiya wa Mwanza, na ikapata nguvu ya Mwl Abdullah Mbanga sahib kuja kushiriki nasi mahubiri kijijini Sungamile, kwa ruhusa ya Amir na Mbashiri MKuu. Kambi hii ilikuwa ni siku 7 kufanya mahibiri, wanajumuiya wa Mwanza tukajipanga kuja na kama kawaida, mzee Saidi Sasamka nae akaahidi kushiriki kikamilifu. Allahu Akbar, kweli mzee akatimiza nia yake. Tena akitoa msisitizo mkubwa kuwa lazima ashiriki kambi ya mahubiri mkoani Shinyanga. Ikumbukwe kuwa wakati huo mkoa wa Shinyanga ulikuwa unasimamiwa na Mwl Musa Kaswezi sahib.

Basi wanajumuiya kutoka Mwanza tukajipanga na kufika mkoa wa Shinyanga na kupokelewa na Mwl Musa Kaswezi sahib, ambapo tuliweka kambi katika mji mdogo wa Kagongwa. Hapo Kagongwa alikuwepo mwanajumuiya mmoja ndugu Farsy Mbaule, ambapo alikuwa ni mwenyeji wetu kwa eneo hilo. Kwa kuwa tulikuwa ni jopo la wanajumuiya wengi, tulimuomba baadhi ya wanajumuiya waweke kambi nyumbani kwake hapo Kagongwa nae akaturidhia. Nakumbuka wanajumuiya waliokaa kwake kwa juma zima walikuwa ni Mzee Sasamka, Mwl Ramadhan Mahmood, Mwl Musa Kaswezi na Mwl Othman AbdulAziz. Idadi ya wanajumuiya waliosafiri kutoka Mwanza kuja walioshiriki kambi ya mahubiri haya mkoani Shinyanga walikuwa ni kama ifuatavyo:-

1. Mzee Saidi Sasamka sahib
2. Mwl Ramadhan Mahmood sahib
3. Mwl Othman AbdulAziz sahib
4. Mzee Salim Thani sahib
5. Bwn Yusuf Mgeleka sahib
6. Mwl Abdullah Mbanga sahib
7. Mwl Musa Kaswezi sahib
8. Yahya Kambaulaya (Yeye alikuja siku ya mwisho kufunga kambi ya mahubiri)

Siku ya mwisho ya kilele chetu cha mahubiri, hapo alikuja ndugu Yahya Kambaulaya sahib na kujumuika nasi kwa mahubiri ya hadhara na kufunga kambi pale kijijini Mondo, nje kidogo ya Manispaa ya Kahama. Hakika, kwa mahubiri hayo kambi ya siku 7, ndio yaliyofanya ikazaliwa Jamaat Ahmadiyya Sungamile. Kazi kubwa sana na mfululizo ilifanywa na wanajumuiya wa Mwanza maana hawakulala kwa kuifikiria Shinyanga, na hapo ndipo tukamuomba tena Amir sahib msaada na muongozo wa kusaidia malezi tawi hilo. Mahubiri haya yaliambatana na sala nyingi za kuomba msaada wa Allah ili kazi hii iliyoanzishwa na kusimamiwa na wanajumuiya ya Mwanza isiishie njiani, na kweli Allah akapokea maombi yetu. Na taarifa rasmi za kila hatua iliyofanywa na kufikiwa, ziliwasilishwa kwa kiongozi wetu Amir sahib maulana Tahiri Mahmood Chaudhry kwa nidhamu zote.

Kwa kupitia hali hizi za wazee na wanajumuiya wa Mwanza, nilijifunza kuwa tunao umuhimu mkubwa sana wa kukaa karibu na wazee. Hawa wazee wetu ni hazina, mapenzi yao kwa Jamaat hayapimiki bali yanakujenga maradufu. Wazee hawana papara, yaani huwezi kuwakuta wazee hawa wakiongea kwa kuikosoa Jamaat yao kwa jambo lolote lile hata kwa nukta, haipo kwao. Wao kazi yao ni kuyafuata mafundisho sahihi ya Masih Aliyeahidiwa, huku wakinisisitizia kudumu kwenye maombi na ibada. Kuanzia hapo, nami katika maisha yangu nikaanzisha mahusiano ya karibu mno ya urafiki na wazee, maana daima wanaikuza imani yako. Wazee hawa wanajua njia nyingi za mahubiri, wanajua namna ya kutuliza joto la kimahubiri la vijana, wazee hawa wa kijamaat ni hazina kubwa...

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Kustawisha Uchamungu wa Kweli na wa Kudumu

Kutoka uk.12

na uchamungu wa kweli. Uchamungu wa kweli hubeba nuru pamoja nao, kama Allah anavyosema:

Enyi mlioamini, mkimcha Allah Atawafanyieni alama ipambanuayo na Atawafutieni makosa yenu ... (8:30).

Enyi mlioamini, Mcheni Allah na mwaminini Mtume Wake; Atawapeni sehemu mbili za rehema Zake na Atawafanyieni nuru mtembee kwayo ... (57:29).
Maana ya Aya hizi ni kwamba:

Enyi mlio amini, Iwapo mtaendelea kuwa thabiti na wenye kumcha Allah, Atakuwekeni tofauti na wengine na tofauti hiyo itakuwa nuru ambayo itaangazia matendo yenu, maneno, uwezo na hisia zenu. Ataangazia akili zenu na mioyo yenu pia. Kutakuwa na nuru machoni mwenu, masikioni mwenu, na katika usemi wenu, na kutembea kwenu na kupumzika kwenu.

Hii ndiyo hali ambayo Muumini na mchamungu wa kweli anatakiwa kuipigania. Ingawa Ramadhani imepita, bado tunaweza kufanya juhudi kufikia hali hii. Na wale tutakaoweza kufanya hivyo tutakuwa wenye bahati kweli kweli.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema: Ni lazima tukumbuke kwamba hii ndiyo enzi ambayo Shetani anafanya kazi hasa, akitumia hila, njama na mbinu zake zote kushambulia. Katika mazingira magumu kama haya, tunahitaji kuonyesha unyenyekevu zaidi kwa Allah, tukitafuta msaada Wake na ulinzi Wake.

Shetani ameweka mitego kupitia njia mbalimbali, kama vile TV, mitandao ya kijamii, na hata kupitia shule za watoto, na kuifanya iwe vigumu kumkwepa isipokuwa kwa neema ya Allāh tu. Wasiwasi wetu wa kimsingi unapaswa kuwa kuwalinda watoto wetu kutokana na mashambulizi ya Shetani, na wazazi wote wawili na Uongozi wa Jamā›at lazima wafanye juhudi za pamoja kuelekea hilo.

Kila mtu mzima, Muahmadiyya anayewajibika lazima ajitahidi kufikia viwango vya juu zaidi vya uchamungu, kwani ni kwa njia hii tu ndipo tunaweza kuvikinga vizazi vyetu vijavyo kutokana na mashambulizi ya Shetani. Badala ya kulegea baada ya Ramadhan, tunapaswa kulenga kuongeza ujuzi wetu zaidi wa Qur›an Tukufu na dini.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema: Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Ni lazima tukumbuke kwamba Dajjāl hakika ni dhihirisho halisi la Shetani ambaye huwapoteza watu kutoka kwenye njia ya haki. Inasemekana kwamba kutakuwa na vita kuu na Shetani katika kipindi hiki, lakini Shetani hatimaye atashindwa. Katika historia ya manabii wote, Shetani daima ameshindwa, lakini huko kulikuwa ni kushindwa kwa muda tu. Kushindwa kwake kabisa kuliamuliwa hatimaye kutatokea mikononi mwa Masihi, na Allāh Ameahidi kwamba Yeye daima atawaweka wafuasi Wake wa kweli kuwa washindi hadi Siku ya Hukumu.

Shetani anakusudia kupigana kwa nguvu zake zote katika siku hizi za mwisho za ulimwengu, lakini ushindi wa mwisho utakuwa wetu.

Masihi Aliyeahidiwa as anasema: Hakika Mwenyezi Mungu atawapa ushindi wafuasi wangu juu ya wapinzani wangu mpaka Siku ya Hukumu.

Masihi Aliyeahidiwa as anasema:
Jueni kuwa kukiri kwa ulimi tu si kitu mpaka kufuatane pamoja na vitendo kwa nia ya moyo wote. Basi mwenye kutenda vitendo sawasawa na mafundisho yangu anaingia katika nyumba yangu iliyoahidiwa na maneno ya Mungu; “***Inniy uhaafidhu kulla man fi-ddari***” –

Yaani – Mimi nitamlinda kila aliyomo katika boma la nyumba yako.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema: Mmekwisha jua kwamba Shetani anayakimbia maneno haya.
“***Laa Hawla walaa Quwwata Illaa Billaahi***”

Yaani - Hakuna nguvu wala uwezo ila kwa kuwezeshwa na Mwenyezi Mungu peke yake.
Lakini tujue kwamba Shetani si mjinga sana hivi kwamba maneno tu yatamfanya akimbie. Maana ya kweli ya hili ni kwamba wale ambao maneno haya yamejikita katika kila chembe ya nafsi zao na daima wanatafuta msaada na usaidizi kutoka kwa Allāh wamehifadhiwa dhidi ya Shetani.
Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Sala ina athari ya sumaku, na inavutia neema na baraka, lakini mpaka mtu aitangulize Qur’ani Tukufu na kuifanyia kazi, maombi yake ni sawa na kupoteza muda tu.
Hadhrat Khalifatul Masih (atba) (atba) amesema:

Vile vile imeelezwa katika Hadith kwamba Sala ndio asili ya ibada. Tukijitahidi kupata dhati hii, tutaweza kutimiza wajibu wetu kwa ajili ya ibada na tutapata ukaribu wa Allāh. Vinginevyo, Sala ya juu juu tu haina thamani.

Kuna watu wasiohesabika wanaokwenda misikitini na kuswali lakini wanafanya dhuluma na uonevu. Mashirika ya kigaidi na wale wanaojiita maulama wanafanya kila aina ya dhulma kwa jina la Allāh na Mtume Wake na wameharibu amani ya dunia.
Khalifa Mtukufu (atba) alisema: Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema: Ni lazima tukumbuke kwamba sala ni ufunguo wa kushinda matatizo yote na kuepusha balaa zote. Hata hivyo, Sala haimaanishi maombi yanayofanywa na watu kama utaratibu tu, badala yake, ni maombi ambayo huufanya moyo wa mtu uyayuke mbele ya Mwenyezi Mungu.

Inapaswa pia kukumbukwa kwamba hatupaswi kulinda sala zetu kwa wazo kwamba Mungu ana haja ya sala zetu. Mungu hahitaji chochote, bali sisi ndio tunamhitaji sana Mungu na ni kwa sababu hii kwamba ni muhimu kwetu kulinda Sala zetu.
Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema: “Sote tumuombe Allāh atupe uwezo wa kuswali kwa ikhlasi.

Na tuwe wale wanaofanya ibada kwa namna ile ambayo inahakikisha uhai wa vizazi vyetu vijavyo. Ni ahadi ya iliyotolewa kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba Dajjal ataangamizwa katika zama zake. Itakuwa ni bahati yetu ikiwa tutajumuishwa katika wale wanaotenda kwa utawa kuwa sehemu ya jumuiya yake.

Kwa ajili hiyo, Masihi Aliyeahidiwa (as) amesisitiza juu ya haja ya kuomba na kuomba kwa kudumu mbele ya Mwenyezi Mungu. Anasema hakikisheni kwamba kwamba hakuna sehemu ya mchana au usiku wenu inayopaswa kukosa kuomba. Tunaomba Allah sote atupe uwezo wa kufanya hivyo.

Mwishoni, Hadhrat Khalifatul Masih (atba) (atba) alisema: “Waombeeni Waahmadiyya wa Pakistani vilevile, Wote Allah awaepushe na hila za wapinzani. Kila Ahmadiyya anayeishi Pakistani anapaswa pia kujiombea. Si jambo la kuomba tu kwa siku tatu au nne au wiki, bali ni muhimu kuomba mfululizo. Fanyeni ahadi ya kuongoza maisha yenu kulingana na amri za Allāh.
Pia kumbukeni kuombea usalama wa Waahmadiyya nchini BurkinaFaso, Bangladesh, Algeria, na kila nchi duniani. Mwenyezi Mungu amlinde kila mmoja wetu na kila Ahmadiyya kutokana na madhara ya maadui zake. Allah Atupe sote uwezo wa kuleta mageuzi safi ndani yetu na kuomba dua zinazokubaliwa na Mwenyezi Mungu. Amiin.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAWAL - DHUL QAD.1444AH | MEI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira*ra* anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume*saw* akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Kustawisha Uchamungu wa Kweli na wa Kudumu

بسم اللہ الرحمٰن الرحیم

Baada ya Kusoma *Tashahhud*, *Tawwudh* na Surah *Al Fatiha, Hadhrat* Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba Leo ni Ijumaa ya mwisho ya Ramadhan na mwezi mtukufu unakaribia kumalizika.

Huenda kulikuwa na baadhi ya watu miongoni mwetu ambao walikuwa wamefanya mipango ya kushiriki katika ibada na kufanya mabadiliko chanya ndani yao wenyewe wakati wa mwezi wa Ramadhan, lakini kwa bahati mbaya hawakuweza kufanya hivyo. Hata hivyo basi, tukumbuke kwamba katika kila Ijumaa unakuja wakati ambapo kila dua inayoombwa ndani yake inakubaliwa.

Sasa kwa vile tunakaribia saa za mwisho za Ramadhan, tunapaswa kuomba kwamba Allah aweze kuyasitiri mapungufu yetu na kutupa nguvu na mwongozo wa kuongoza maisha yetu kwa mujibu wa vile Apendavyo kutoka kwetu tuwe. Khalifa Mtukufu (atba) alisema: Iwapo tutaendelea kujitahidi kuishi kwa



*Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano*atba *akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 21 April, 2023.*

Kustawisha Uchamungu wa Kweli na wa Kudumu

uchamungu kuanzia Ijumaa moja hadi nyingine, na hivyo hivyo kutoka Ramadhan moja hadi Ramadhan nyingine, basi haitatunufaisha sisi tu bali na vizazi vyetu vijavyo pia. Kwa njia hii, tutafikia lengo la kweli ambalo Masihi Aliyeahidiwa (as) alianzisha Jamaat hii. Kupata Taqwa ndio lengo ambalo Masihi Aliyeahidiwa (as) amelisisitiza sana.

Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa ili viwango vya uchamungu wetu viinuliwe. Wakati mmoja, alisema: Nimetumwa ili kwamba zama za ukweli na imani zirudi na mioyo ijazwe na uchamungu, na haya ndiyo malengo ya mwisho ya ujio wangu. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema: Kwa mujibu wa bishara za Mtukufu Mtume (saw), zama za Masihi Aliyeahidiwa (as) zitadumu hadi Siku ya Hukumu. Sasa ni juu ya wafuasi wake kujitahidi kufikia viwango vya juu vya ibada huku wakibaki imara juu ya ukweli. Lakini lengo hili haliwezi kufikiwa kwa mwezi mmoja tu wa ibada au matendo mema, bali ikiwa tutaendelea na ibada zetu, tutakuwa miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu alimwambia Masihi Aliyeahidiwa as, “Mimi ni pamoja nawe na wale unaowapenda.»

Kwa hivyo kama tunatumia maisha yetu kwa namna hii, kupitia matendo yetu, tutawaeleza wanadamu kwamba kama wanataka kuanzisha uhusiano ulio hai na Mwenyezi Mungu, basi njooni mumpokee mtumishi huyu mwaminifu wa Mtukufu Mtume (s.a.w).

Ucha Mungu wa kweli ni nini? Na mtu anakuwaje anaposhika uchamungu wa kweli? Na vipi Allah huwatendea wale wanaoshika uchamungu wa kweli?

Kuhusiana na hayo, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: Ujinga hauwezi kuambatana

Endelea uk.11



MWITO KWA MFALME
Dawat-ul-Amir

Mwito kwa Mfalme ulichapishwa kwa mara ya kwanza katika Kiurdu mwaka 1926 na kisha kutafsiriwa katika Kiajemi kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mtawala wa Afghanistan, Amanullah Khan. Miaka miwili au zaidi kabla ya kitabu kilitungwa, Waahmadiyya watatu wa Afghanistan walikuwa wamepigwa mawe hadi kufa kwa amri ya Amanullah Khan. Msiba huu matukio alifanya hivyo muhimu kwamba massage, malengo na mantiki ya Jumuiya ya Ahmadiyya inapaswa kufafanuliwa kwa uangalifu maalum wa Mfalme. Madhumuni ya kitabu kilikuwa kimfikishie Mola Mtukufu ukweli akaunti ya imani na mafundisho ya Harakati na madhumuni ya kuanzishwa kwake. Ilikusudiwa pia kukanusha mashtaka ya uwongo ambayo yalitolewa dhidi ya harakati na miungu halisi na kupinga madai yasiyo na msingi kufanywa dhidi ya harakati. Matukio na kitabu sasa ni cha historia, lakini kitabu chenyewe kinaendelea kukua ndani athari na ushawishi.

Inabainisha bishara za Mtukufu Mtume*saw* zilizotajwa katika vitabu vya Hadithi na kuchunguza maamlisho yake ya kweli. Inatoa ufafanuzi wa madai ya Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya na kutoa maelezo ya sababu katika msaada wao. Inaendelea kuanzisha, kwa misingi ya Quran Tukufu na Hadithi za Mtukufu Mtume*saw* kwamba yule kiongozi wa kiroho ambaye ujio wake alikuwa ametabiriwa tayari ametokea katika nafsi ya Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya, na kusisitiza kwamba, wokovu wa wanadamu upo katika kumkubali na kumfuata.

Je, Wajua?

Je wajua, kuwa Mwaka 2018 NASA (Shirika la anga la Marekani) lilituma chombo kilicholengwa kufika katika jua. Chombo hicho kinaweza kuhimili joto la 2,500°F (1,377°C). Tarehe April 28, 2021. Chombo hicho kiitwacho Parker Space Probe kilifika katika anga ya jua na kupiga picha. Mpaka leo hii chombo hicho kimezunguka jua mara kadhaa na kinaendelea kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu Jua.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com